



UNIVERSITY OF UTAH
SCHOOL OF MEDICINE

Kauli ya Haki

za Mhusika katika Utafiti

Kila mtu ana haki. Watafiti katika Chuo Kikuu cha Utah wanataka ufahamu haki zako.

Wewe ama jamaa yako mna haki ya:

Kufahamishwa kwa nini utafiti unafanywa.

Kufahamishwa tofauti katika huduma zako za kawaida na jinsi zinavyofanana.

Kufahamishwa hatari na matatizo yoyote yanayoandamana.

Kufahamishwa iwapo kuna manufaa yoyote kwako kwa kushiriki katika utafiti na manufaa yenyewe.

Kufahamishwa kuhusu chaguo zilizopo, manufaa na hasara.

Kufahamishwa huduma zozote za afya zilizopo iwapo kuna majeraha ama matatizo yanayotokana na kushiriki katika utafiti.

Kuwa na muda wa kuwaza iwapo ungependa kushiriki.

Kupewa fursa ya kuuliza maswali, kabla na wakati wa utafiti.

Kuamua KUTOSHIRIKI katika utafiti wakati wowote. Haki zako katika huduma za afya hazitaathirika iwapo utaamua kutoshiriki katika utafiti.

Kufanya uamuzi bila kushurutishwa.

Kupewa nakala ya fomu ya kukubali iliyotiwa saini.



Iwapo una maswali au masuala yoyote kuhusu haki zako, ma haki za jamaa yako, tafadhali wasiliana na daktari wako wa utafiti.

Unaweza pia kuwasiliana na Halmashauri ya Utathmini wa Taasisi katika Chuo Kikuu cha Utah (IRB) katika
(801) 581-3644

Ama Wakili wa Mhusika katika Utafiti katika (801) 581-3803.

